

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA.**

SHULE YA SEKONDARI BUDEKWA,  
S.L.P. 11,  
MASWA.

15/12/2020

**KUMB NA: MDC/SED/JI F.1/2020**

MZAZI / MLEZI WA: .....

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SEKONDARI YA KUTWA BUDEKWA.**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka wa masomo 2021. Shule ya Sekondari Budekwa ipo umbali wa Km 45 kutoka mjini Maswa. Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021** siku ya jumatatu. Na mwisho wa kuripoti ni **18/01/2021**

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.**

**2.1 SARE ZA SHULE.**

**I. WAVULANA**

- Suruali mbili nyeusi marinda yasiyozidi mawili na mifuko mitatu isiyo ya kubandikwa (zitakaguliwa hapa shuleni)
  - Shati mbili nyeupe tetron zenye mikono mifupi.
  - Viatu vyeusi visivyo na soli ndefu au nene na visiwe visiwe na urembo
  - Sweta rangi ya kijani
  - Soksi ndefu jozi mbili nyeusi
  - Tai nyeusi
  - Mkanda wa ngozi usiwe na chuma kikubwa
- Tanibih:** Suruali za dingrees au jeans ni marufuku.

**II. WASICHANA**


- Sketi mbili nyeusi zenye rinda boksi ndefu mpaka kisiginoni
- Shati mbili nyeupe tetron zenye mikono mifupi.
- Viatu vyeusi visivyo na soli ndefu au nene na visiwe na urembo
- Sweta rangi ya kijani
- Soksi ndefu jozi mbili nyeupe
- Tai nyeusi
- Rangi ya Hijabu ifanane na sare za shule

**2.2 MAVAZI YA MICHEZO**

WASICHANA: Sketi nyeusi, raba nyeusi na T- Shirt ya bluu

WAVULANA: kaptula nyeusi, raba nyeusi na T-Shirt ya rangi ya bluu

KWA WOTE: Suruali (truck) na T-Shirt "mikono mifupi" rangi ya bluu

  
MKUU WA SHULE  
SHULE YA SEKONDARI BUDEKWA  
MASWA

### **2.3 MAHITAJI YA TAALUMA**

- i) Mfuko wa kubebea madaftari (school bag)
- ii) Mathematical set (mkebe wa zana za hisabati)
- iii) Kalamu za wino na penseli
- iv) Rula na kifutio
- v) Dictionary ya kingereza kwa kingereza
- vi) Madaftari (counter book 2 quire) 10

### **3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu No 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo inayoyolewa na Wizara ya Elimu Sayansi, Teknolojia na Ufundi nchini. Sheria na kanuni za shule ni:-

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya darasa kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya juu kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wa uanafunzi wako katika shule hii.
- e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
- f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
- h) Kutunza mali za umma.

### **4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.**

- a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospital ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni (FOMU A)
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai (FOMU B)

### **5.0 MWISHO**

Shule hii ni ya kutwa, hivyo mwanao baada ya masomo atakuwa akirejea nyumbani au sehemu utakayokuwa umempangishia. Ufikapo shuleni tafadhali ripoti ofisi ya mkuu wa shule

5.1 tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo hayo na kuyatekeleza kikamilifu

**KARIBU SANA BUDEKWA SEKONDARI**



**MAJIGE NGANGALA  
MKUU WA SHULE.  
(0627 85 17 74)**

**MKUU WA SHULE  
SHULE YA SEKONDARI BUDEKWA  
MA SWA**

**FORM 'A'**  
**MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING**

BUDEKWA SECONDARY SCHOOL  
P.O. BOX 11,  
**MASWA.**

**DATE:** .....

TO THE MEDICAL OFFICER,  
.....  
.....  
.....

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please examine the above mentioned boy as to / his fitness for student in this school. (This form must be filled in by the government medical officers)

Student's full name : .....  
Present age : .....  
Blood test : .....  
Stool Examination : .....  
T. S. Test : .....  
Asthma : .....  
Eye disorder : .....  
Ear disorder : .....  
Norse disease : .....  
Anemia : .....  
Chest : .....  
Operations : .....  
Serious accidents : .....  
Pregnancy : ..... (in case of female).

**ADDITIONAL INFORMATION EG. Physical or impairment, Chronic or family disease etc :** .....

I certify that I have personally examined miss ..... and found him/fit to passed further study.

**Signature** .....

**Designation** .....

**Official Stamp** .....

  
MIKUU WA SHULE  
SHULE YA SEKONDARI BUDEKWA  
MASWA

## FOMU 'B'

### MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi .....
  2. Tarehe ya kuzaliwa .....
  3. Uraia ..... Dini ..... Dhehebu .....
  4. Kabila ..... Jinsia .....
  5. Shule ya Msingi ..... namba ya Mthani .....
  - Kata ..... Tarafa .....
  6. Jina kamili la baba ..... Kijiji .....
  - Kata ..... Tarafa .....
  7. Jina kamili la mama ..... / amefariki .....
  - Kijiji ..... Kata ..... Tarafa
  8. Jina kamili la Mlezi (kama hana mzazi) .....
  9. Uhusiano na Mlezi.....
  10. Kazi ya Baba / Mlezi .....
  11. Jamaa katika familia
    - Idadi ya kaka .....
    - Idadi ya dada .....
    - Yeye ni wa ngapi katika familia .....
  12. Je, Uwapo masomoni hapa utakuwa unaishi nyumbani kwenu / nyumba ya kupanga / kwa ndugu au jamaa? .....
  - Kama ni ndugu au jamaa anaitwa? .....
  13. Nathibitisha kuwa mwanangu atazingatia sheria taratibu za shule.
- Jina : ..... Saini : .....
- Simu Na: ..... Tarehe: .....

  
MKUU WA SHULE  
SHULE YA SEKONDARI BUDEKWO  
MA S WA